# EE MSALABA WA MWOKOZI

Bunghart




1. Ee msalaba wa Mwokozi mpenzi wa moyoni, udaraja la kuvuka shimo la motoni,
   Kwa kupanda uwinguni ndiwe ngazi ndefu, kwako tunatumaini sisi wakosefu.

2. Ee msalaba twakusifu mti wa baraka, Wewe waonesha njia tukiona shaka,
   Mbingu zikigongwa nawe mlango wafunguka, Tuinulie moyo kwako neema itashuka.

3. Ee msalaba Mtakatifu pote uwe nami, Ndiwe mti tuushike kamwe hatuzami,
   Ndiwe kiwi funga moyo haingii shetani, Kweli tu wokovu wetu uko msalabani.